

***‘Kiongozi Mtumishi’ Dk. Syreeta McTier Atunukiwa  
Kama Mtaalamu wa Pili wa Usaidizi wa Kielimu wa  
DCSD wa Mwaka***

Dk. Syreeta McTier alilelewa katika mazingira ya kutumikia wengine tangu siku alipozaliwa. Kwa hivyo, haikushangaza kwamba alisomea ualimu ili kuhudumia na kuelimisha watoto. Kujitolea kwake katika huduma kulimfanya atajwe kama Mtaalamu wa Pili wa Usaidizi wa Kielimu wa Wilaya ya Shule ya Kaunti ya DeKalb County (DCSD) wa 2023–2024 wakati wa Tuzo za 10 za Chuo cha Ubora wa Kielimu za Kila Mwaka katika msimu uliopita wa mapukutiko. Dk. McTier alitoa shukrani kwa heshima hii ya kifahari aliyopokea kama mwalimu mkuu msaidizi katika Shule ya Smoke Rise Elementary.

“Ni baraka ya kweli kupokea tuzo hii tukufu ambayo inatambua ubora wa kazi, ari na michango yangu kwa Wilaya ya Shule ya Kaunti ya DeKalb,” alisema.

Kwa miaka 21, Dk. McTier amekuwa mwalimu katika Shule za Kaunti ya DeKalb. Alitiwa moyo kuwa mwalimu na mamake, aliyekuwa mwalimu mahiri na nguzo katika jamii ya Compton, California kwa zaidi ya miongo mitatu. Urithi wa mama yake ulimfundisha kwamba walimu wana uwezo wa kuathiri wanafunzi na familia zao kwa vizazi vingi vijavyo.

“Wakati wa kazi yake ya miaka 34, alifundisha watoto na wajukuu wa wanafunzi wake wa zamani. Mama yangu ndiye kielelezo changu na msukumo wangu kama mwalimu,” alisema Dk. McTier. “Kwa sababu ya mfano mzuri wa mamangu, nilichagua elimu kama njia yangu ya kutoa huduma. Heshima hii ya kipekee ni ushuhuda wa ushawishi wake ninapofuata nyayo zake.”

Dk. McTier alianza taaluma yake kama mwalimu katika Shule ya Jolley Elementary, ambako alihudumu kwa miaka sita. Baada ya hapo, akawa mwalimu mkuu msaidizi katika Shule ya Robert Shaw Traditional Theme na alihudumu huko kwa miaka minne. Baada ya hapo, aliamia Shule ya Smoke Rise Elementary, ambapo amekuwa kwa miaka 11. Alisema kuwa anapenda kuwa sehemu ya jamii ya shule ya Smoke Rise Elementary.

“Mazingira yetu ya shule ni yenye upendo na ya kujali, na yanazingatia ukuaji na ufaulu wa wanafunzi,” alisema. “Watu hawa wa ajabu, ikiwa ni pamoja na wanafunzi, walimu, wafanyakazi, walimu wakuu, wasimamizi, wazazi, familia, na wanajamii, hufanya Shule ya Smoke Rise Elementary kuwa mahali pa kipekee pa kufanya kazi, kujifunza, na kukua. Ingawa kila mmoja wetu ana jukumu tofauti, tunafanya kazi pamoja kwa ushirikiano kwa ajili ya ufaulu wa wanafunzi.

Mnamo mwezi Januari, Smoke Rise Elementary iliandaa sherehe ya kumheshimu Dk. McTier na wafanyakazi wengine wa shule wa mwaka. Wakati wa hafla hiyo, Meya Frank Auman wa Jiji la Tucker alimpa Dk. McTier barua ya kumpongeza kwa kuteuliwa kuwa Mtaalamu wa Pili wa Usaidizi wa Kielimu wa DCSD wa Mwaka.

“Ilikuwa sherehe ya dhati na ya kukumbukwa kwa watuzwa na wapendwa wetu,” Dk. McTier alisema.

Mkuu huyu msaidizi bora ana jukumu muhimu katika kushirikiana na mwalimu mkuu, walimu, wafanyakazi, wanafunzi, wazazi na wanajamii ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji na kuboresha ukuaji na ufaulu wa wanafunzi. Sehemu anayopenda zaidi ya kazi yake ni kusherehekea ukuaji wa wanafunzi. Wakati atakapostaafu, Dk. McTier anatumai kwamba urithi wake utakuwa kwamba aliongeza thamani kwenye hali za kielimu na kitaaluma kwa wengine na kuleta athari chanya katika maisha yao.

“Urithi wangu ni kuwasaidia wengine kufikia kusudi lao, kujumuisha upendo na kuhamasisha ubora,” alisema.

**XXX**